# Athari za Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili

Aginiwe Nelson Sanga
Chuo Kikuu cha Dodoma

**Ikisiri**

Mkengeuko wa ujumi katika uga wa fasihi hurejelea hali ama ya mwandishi au msomaji kutovutiwa kuandika au kusoma kazi zinazohusu maisha halisi ya tabaka lake au utamaduni wa jamii yake. Badala yake hugeuka na kuvutiwa kuandika au kuzisoma kazi za fasihi za tabaka au jamii zenye utamaduni usioelekeana na wake (Sanga, 2018). Katika makala hii zimechunguzwa baadhi ya hadithi fupi andishi kutoka katika magazeti ya *HabariLeo*, *Nipashe* na *Mwananchi* ya mwaka 2008 hadi 2014, ambazo ni sehemu ya kipindi cha utandawazi. Hadithi fupi andishi za Kiswahili za kipindi hiki cha utandawazi, zimekengeuka kiujumi kutoka kwenye zile za asili ambazo ni hadithi fupi simulizi. Ukengeufu umejikita katika namna hadithi zinavyotungwa, zinavyohifadhiwa, zinavyoifikia hadhira, masuala yanayojadiliwa, mahali na wakati wa kusomwa. Hali hiyo imeufanya utanzu huu kuwa na sifa zinazokaribiana na riwaya kiasi cha kupoteza utambulisho wake. Aidha, hadithi fupi za sasa zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na usasa pamoja na umiji, jambo lililosababisha utanzu huu kuibagua hadhira, kirika na kimaeneo. Vilevile, maudhui ya hadithi fupi andishi yameonekana kuwa na mvuto kwa vijana wa mjini kuliko wazee. Hii ni kwa sababu visa vyake vingi na matukio huhusu mapenzi ya kisasa, masuala ya uhalifu, ugaidi na maisha ya wanafunzi wa vyuo vikuu. Matukio haya yanawagusa zaidi vijana kuliko wazee. Jamii za sasa za Kiafrika zimekengeuka kiujumi na kuvutiwa na mambo yanayofungamana na utamaduni wa Kimagharibi kuliko wa Kiafrika.

## 1.0 Utangulizi

Utandawazi ni mchakato wa kijamii ambao unaruhusu kuondolewa kwa vikwazo vya kijiografia katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na katika miundo ya kijamii na kiutamaduni ambapo watu huwa wanaelewa na huwa sehemu katika mabadiliko hayo (Waters, 2001). Kipindi cha utandawazi kimesababisha kuwapo kwa mabadiliko makubwa katika nyanja muhimu za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Mabadiliko hayo yametokana na maendeleo ya kiwango cha hali ya juu cha

kiteknolojia. Fasihi ni zao la jamii na mabadiliko yanapojitokeza katika jamii fasihi nayo huakisi mabadiliko hayo. Hadithi fupi ni utungo wa kinathari unaosimulia kisa au tukio kwa kujigeza katika ufundi wa kutumia lugha kwa ubanifu. Ubanifu huo hudhihirika katika wahusika, mandhari, wakati na visa vinavyosimuliwa. Usimulizi katika utanzu huu hauna utondoti wa kimaelezo kama wa riwaya, kinachotawala katika hadithi fupi ni mada kuu inayosimuliwa. Utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili kama utanzu mmojawapo wa fasihi andishi, nao umekumbwa na mabadiliko hayo kifani na kimaudhui kwa kiasi cha kukengeuka kwenye ujumi wa Kiafrika. Ujumi wa Kiafrika ni dhana inayojumuisha mtazamo na tajiriba katika kuhakiki, kutambua, kutathmini uzuri au ubaya, ubora au udhalili, uhasi na uchanya wa kazi za sanaa za Waafrika kulingana na hali halisi ya ulimwengu wa Waafrika. Kwa Waafrika, sanaa haipo kwa kukidhi malengo yake yenyewe tu, bali hata hali halisi zilizopo katika mazingira na miktadha mbalimbali ya kijamii. Mkengeuko wa ujumi katika uga wa fasihi hurejelea hali ama ya mwandishi au msomaji kutovutiwa kuandika au kusoma kazi za fasihi zinazohusu maisha halisi ya tabaka lake au utamaduni wa jamii yake. Badala yake hugeuka na kuvutiwa kuandika au kuzisoma kazi za fasihi za tabaka au jamii yenye utamaduni usioelekeana na jamii yake (Sanga, 2018).

Katika makala hii zimechunguzwa hadithi fupi andishi kutoka magazeti ya *HabariLeo*, *Nipashe* na *Mwananchi* ya Mwaka 2008 hadi 2014. Nadharia ya Umaksi na Ujumi Mweusi ndizo zimeongoza uchambuzi wa hadithi fupi andishi teule. Data za makala hii zilikusanywa kupitia mbinu za mahojiano, uchanganuzi matini na vikundi lengwa. Uchambuzi umebaini kuwa hadithi fupi andishi za Kiswahili za kipindi cha utandawazi zimekengeuka kiujumi kutoka zile za asili ambazo ni hadithi fupi simulizi. Namna hadithi za utandawazi zinavyotungwa, zinavyohifadhiwa, zinavyowafikia hadhira, masuala yanayojadiliwa, mahali na wakati wa kusomwa vimepokea mabadiliko makubwa. Mabadiliko yaliyojitokeza katika hadithi fupi andishi za Kiswahili yanakwenda sambamba na kukengeuka kiujumi kwa utanzu huu. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu nne: Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, sehemu ya pili inaelezea kwa ufupi namna mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika ulivyojitokeza katika hadithi fupi andishi za Kiswahili. Sehemu ya tatu inafafanua athari zilizotokana na mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi andishi za kipindi cha utandawazi na sehemu ya nne ni hitimisho.

## 2.0 Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili

Wataalamu wa Fasihi ya Kiswahili wanakubaliana kuwa hadithi fupi andishi za Kiswahili ni kama mwendelezo wa hadithi fupi simulizi (Wamitila, 2010; Samwel, 2012, 2013). Kiuamilifu na kimaudhui hadithi fupi simulizi zilipewa nafasi kubwa

katika jamii za Waafrika katika kufunza, kuburudisha, kuelimisha na kuwakuza vijana kiakili, kijamii, kitabia, kiroho na kimaadili. Lakini tunapozisoma hadithi fupi andishi za sasa zinaonekana kukengeuka kutoka hadithi fupi simulizi. Hata hivyo, makala hii imejikita katika uchunguzi wa athari zilizojitokeza kwa upande wa utanzu wa hadithi fupi baada ya kukengeuka kwa vipengele vya ujumi wa Kiafrika katika upande wa maudhui na fani.

Utandawazi umeonekana kuwa ni mfumo wenye mchangamano na mkinzano wa masuala mengi. Masuala hayo ni yale yenye athari chanya na hasi kwa jamii zote za mataifa tajiri na maskini. Wapo wataalamu wanaouona utandawazi kuwa ni nguvu isiyoweza kukwepwa au kuzuiwa na jamii yoyote ile na kwamba utandawazi una manufaa ya kiuchumi kwa jamii zote za ulimwengu (Dollar na Kraay, 2001). Upande mwingine wapo wanaoona utandawazi ndicho chanzo cha matatizo makubwa yanayoukumba ulimwengu wa sasa kama vile ugaidi, kuenea kwa magonjwa kama ebola, UKIMWI, ndoa za jinsia moja, madawa ya kulevya, njaa, vita, kuporomoka kwa uchumi wa baadhi ya mataifa na kusambaa kwa imani mbalimbali potofu (Shepard na Hayduk, 2002).

Athari za teknolojia ya kisasa zimeufanya utandawazi kuwa na sura mpya ukilinganisha na hali halisi ilivyokuwa katika jamii nyingi za dunia kabla ya utandawazi. Vizuizi vya asili vya umbali halisi na muda wa kuyafikia maeneo kijiografia vimepunguzwa kwa kiasi kikubwa. Gharama za mijongeo au kusafiri kwa habari, watu, bidhaa, mitaji, ujuzi, huduma na sanaa zimekuwa zikipungua siku hadi siku. Urahisi wa mawasiliano na mahusiano ya jamii za ulimwengu yametoa fursa ya kupanuka kwa biashara na mahusiano ya utamaduni baina ya jamii za mataifa ya dunia nzima. Hata hivyo, mataifa yaliyoendelea yaani mataifa yenye uchumi wa viwanda ndiyo yanayonufaika na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupitia utandawazi. Mataifa hayo ni vinara wa uvumbuzi na utumiaji wa teknolojia hiyo ya kisasa. Wakati huo mataifa maskini yaliyo mengi hususani yaliyopo Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, yamekuwa waathirika wa utandawazi. Mataifa ambayo hayajaendelea kiviwanda yamejinasa kwenye mduara wa utelezi unaochochewa na umaskini, ujinga, migogoro, uongozi mbaya, matatizo ya mazingira na uchumi unaotegemea vyanzo vya aina moja tu, hususani malighafi. Mataifa maskini yanadaiwa madeni makubwa na mataifa yaliyoendelea kiviwanda kiasi kwamba hata bei za malighafi yanayozalisha kuyauzia mataifa yaliyoendelea kiviwanda ni za chini sana. Hali hiyo, huziweka nchi maskini kuwa katika dimbwi la utegemezi katika nyanja zote za maisha. Kwa jumla, mahusiano ya mataifa haya yana athari za kitabaka. Athari hizo hazikukomea katika maeneo hayo pekee yaliyoyatajwa, zimeuathiri hata utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili.

## 3.0 Athari za Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili

Mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika utanzu wa hadithi fupi andishi katika kipindi hiki cha utandawazi umeleta athari nyingi katika utanzu husika. Athari hizo zipo katika namna mbalimbali: Mosi, kuna athari chanya na hasi. Athari chanya za mkengeuko wa ujumi zinatokana na mabadiliko yaliyosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kisasa katika utanzu. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuongezeka kwa njia bora za kuusambaza na kuhifadhi utanzu huu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili. Pia, kupanuka au kuongezeka kwa eneo na hadhira, na urahisi wa kufikiwa na hadhira mara wanapohitaji. Athari hasi zilizojitokeza kwa utanzu huu ni kupungua kwa uthamani wake katika jamii, kudondoshwa kwa mambo muhimu ya utamaduni wa Mwafrika katika utanzu na kuyaingiza ya Kimagharibi. Pili, ni athari za kimaudhui na za kifani katika utanzu. Athari za mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi andishi za Kiswahili zilizojadiliwa katika makala hii ni za kimaudhui na kifani katika vipengele vya: utambulisho wa utanzu, wahusika, msuko wa matukio, upokezi kwa jamii, uhifadhi na ufikiwaji na mkanganyiko katika mitazamo.

### 3.1 Maudhui Mapya na Yasiyozoeleka

Maudhui ya hadithi fupi simulizi yalilenga kukuza na kudumisha ushirikiano, utu, utii na adabu, ushujaa na imani za dini. Hata hivyo, hadithi hizo zilikuwa zinafungamana na jamii ndogo ya eneo fulani kama vile wafugaji, wakulima, wavuvi, wafinyanzi au wahunzi. Utanzu wa hadithi fupi enzi hizo ulipewa jukumu kubwa la kuwaelimisha wanajamii juu ya mambo mbalimbali muhimu kwa maendeleo ya jamii. Maudhui ya kipindi cha utandawazi yanasawiri mahusiano ya kiutandawazi, yanayohusu jamii za mataifa mbalimbali ya dunia. Masuala mtambuka ya kidunia ndiyo yaliyotawala katika hadithi fupi andishi za Kiswahili za sasa. Kwa mfano, masuala ya utumiaji wa dawa za kulevya, mahusiano ya kimapenzi yenye uhuru usiokuwa na mipaka, ubinafsi na usasa.

Baadhi ya maudhui yaliyojitokeza katika hadithi zilizochambuliwa katika magazeti teule yana mwelekeo wa fasihi ya ulimwengu. Kwa mfano, katika hadithi ya *Utata Mtupu* iliyoandikwa na Fridolin katika *Nipashe* tar. 6-17/6/2013 na *Oh Ramla* iliyoandikwa na Matola katika *Nipashe* tar. 3-6/4/2012 zinazungumzia mahusiano ya mapenzi yasiyo ya kawaida katika jamii za Waswahili. Katika hadithi ya *Utata Mtupu* Herrieth amemwoa Frank na kumweka ndani huku akimpatia matunzo yote. Jambo hilo siyo la kawaida kwa utamaduni wa Waswahili kwa mwanamke kumwoa mwanamume. Mwandishi anasimulia:

> Sasa kitendo cha kumpiga kimemkasirisha sana mchumba wake kiasi akafikia kumfukuza kwenye nyumba aliyompangishia kule Sinza. Toka hapo mchumba wake amebadili namba zake zote za simu, jambo lililomfanya huyu bwana ashindwe kuwasiliana naye ili aombe msamaha. Sasa mbaya zaidi ni kuwa yule msichana aliyefumwa naye ameamua kukatisha uhusiano wake na rafiki yangu na hataki kumwona (*Nipashe*, 13/06/2013).

Katika nukuu hii Dennis rafiki wa Frank anamwelezea Daktari historia ya ugonjwa wa Frank ambaye amelazwa hospitali akiwa amepoteza fahamu. Amefikia hatua ya kuugua ugonjwa wa sonona kutokana na mchumba wake Herrieth kusitisha huduma alizokuwa akimpatia. Alikuwa amempangishia nyumba, akimnunulia nguo, chakula na kumpatia huduma zote za msingi. Mahusiano ya kimapenzi ya Frank na Herrieth yalianza wote wakiwa wanachuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Herrieth alikuwa mwaka wa tatu na Frank mwaka wa kwanza. Baada ya kumaliza masomo Herrieth alipata kazi, ambapo akaamua kumtoa mchumba wake katika 'hostel' za Chuo na kumpangishia chumba Sinza. Frank alikuwa ni kijana asiyeridhika na mpenzi mmoja, siku alipofumaniwa akiwa na msichana mwingine katika chumba alichopangishiwa, ukawa ndio mwisho wa mapenzi na hao wapenzi wake wote. Kuugua kwa Frank ugonjwa wa sonona ni uthibitisho wa wazi kuwa huyu kijana alikuwa katika mtanziko wa namna atakavyoishi baada ya kusitishwa kwa misaada kutoka kwa mpenzi wake Herrieth. Jambo hili kwa asili katika jamii za Kiafrika halikuwapo, ujumi wa mwanamume ulikuwa umejikita katika tabia za ushababi.

Pia, katika hadithi ya *Oh Ramla* tunamwona Fikiri akifanya jaribio la kumbaka mdogo wake Ramla. Ramla alikuwa ni mtoto wa mama mkubwa wa Fikiri. Ramla alihamishwa shule kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam na mama yake mdogo (mama Fikiri) ili akaendelezwe kielimu. Kinyume cha mambo ni kwamba shuleni hakupelekwa, aliishia kuwa msichana wa kazi katika nyumba hiyo pamoja na kubakwa na kaka yake, Fikiri. Misingi ya ujumi wa jamii za Kiafrika kwa asili imejikita katika kujali thamani za utu, udugu, ushirikiano na kuheshimiana. Izingatiwe kuwa ujumi ni tawi la falsafa linalojishughulisha na masuala kama ya ladha, uzuri, uwi, ubora, udhalili, uhasi na uchanya, vitendo alivyotendewa Ramla na familia ya mama yake mdogo siyo vya kiutu na ni kinyume na ujumi wa Kiafrika.

Maudhui ya hadithi nyingi zilizochunguzwa katika utanzu huu yalionekana kuwahusu vijana wa jamii ya mijini na wakati huo watu wa vijiji na wazee wakikosa nafasi. Ikumbukwe kuwa utambaji wa hadithi fupi kabla ya utandawazi ulihusisha makundi yote katika jamii na utendaji ulifanyika kwa ushirikiano. Aidha, mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi andishi umesababisha kuwapo

kwa maudhui ya kidunia katika utanzu huu. Maudhui haya kwa sehemu kubwa yamebeba itikadi za kibepari ambapo ubinafsi umekuwa ukitukuzwa na kukuzwa. Hivyo, uzuri wa kiujumi kwa misingi ya upebari huangaliwa katika masuala ya kibinafsi zaidi. Hili ni kinyume na maudhui yaliyochagizwa na utanzu wa hadithi fupi simulizi kabla ya utandawazi, ambapo kwayo uzuri wa kiujumi ulitazamwa kupitia ushirikiano, utu, kuheshimiana na kusaidiana.

### 3.2 Kufifisha Utambulisho wa Utanzu

Mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika umefifisha utambulisho wa utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili. Sifa za utanzu huu kama zilivyokuwa zikibainishwa hapo mwanzo kwa sasa zimebadilika. Hili limejitokeza karibia katika tanzu zote za fasihi andishi. Utanzu wa hadithi fupi simulizi za Kiswahili kabla ya utandawazi ulikuwa unatambwa kwa ushirika kwa maana ya kwamba fanani na hadhira walionana ana kwa ana na kushirikiana katika utambaji. Hali ilivyo kwa sasa ni kwamba utanzu wa hadithi fupi andishi umekuwa ni wa kibinafsi, mtunzi anakuwa peke yake na msomaji anahitaji muda wa faragha ili azame katika hadithi anayosoma.

Aidha, utanzu huu ulitambulika hapo mwanzoni kuwa na sifa ya kueleza wazo kuu moja linalotawala hadithi nzima, lakini hadithi nyingi za sasa zinakuwa na mwingiliano wa mambo mengi katika hadithi moja. Kwa mfano, katika hadithi ya *Utata Mtupu* tuliyoichunguza, masuala ya mapenzi, usaliti na elimu yamepewa nafasi sawa katika hadithi. Sifa nyingine iliyokuwa ikielezwa hapo awali kuwa ni ya utanzu huu inahusiana na masuala ya wahusika. Utanzu huu ulijulikana kuwa na wahusika wachache na kuwa na muundo sahili. Mathalani, Madumulla (2009:96) anaeleza kwamba hadithi fupi za kisasa zingepaswa kuitwa riwaya fupi kwa kuwa uzito wake umebebwa katika kipengele cha ubunaji na usawiri wa matukio unaokileta kijitanzu hiki karibu kabisa na uhalisi wa maisha.

Tunapozifafanua sifa za riwaya kwa kulinganisha na sifa za hadithi fupi ni wazi kuwa kuna kufanana kwa kiasi kikubwa kuliko kutofautiana kwake. Jambo hili limezua mkanganyiko miongoni mwa wataalamu wa fasihi kuhusu utambulisho wa utanzu huu. Baadhi ya wahadhiri wanaofundisha fasihi wanapoainisha tanzu za fasihi andishi, utanzu wa hadithi fupi andishi huchukuliwa kama sehemu ya riwaya (Samwel, 2012).

Makala hii inaona mkanganyiko huu umesababishwa na mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika utanzu husika, baada ya kukabiliwa na mabadiliko ya kiutandawazi. Utanzu wa hadithi fupi andishi unapaswa kupewa uzito wa kipekee na wadau wote wa fasihi pengine kuliko utanzu wa riwaya kwa kuwa bado una nafasi kubwa ya kuisaidia jamii ya Waafrika hususani Waswahili kutokana na sifa yake ya kueleza mambo kwa muhtasari au mbano. Wanajamii wa sasa

wanakimbizana na shughuli mbalimbali za maisha, hawana nafasi ya kusoma hadithi ndefu kama za riwaya, hadithi fupi zingetumiwa vizuri zingeweza kuwa mwafaka kwa jamii yetu katika kipindi hiki cha utandawazi. Uchunguzi umeonesha kuwa hadithi fupi simulizi zilikuwa zikitegemewa sana na jamii za mwanzo kama nyenzo ya kufanikisha masuala mbalimbali katika maisha kuliko ilivyo kwa hadithi fupi andishi za wakati wa utandawazi.

**3.3 Usawiri Usiozoeleka wa Wahusika**

Wahusika ni kipengele cha muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Wahusika huwa ni kielelezo cha utamaduni wa jamii, hubeba maudhui ya kazi ya fasihi. Wahusika pamoja na majina, tabia na mavazi yao husaidia kueleweka kwa maudhui na huongeza mvuto katika kazi ya fasihi. Mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika umeathiri kipengele cha wahusika katika hadithi fupi andishi za Kiswahili. Wahusika wa hadithi fupi simulizi aghalabu huwa ni wahusika wakwezwa na bapa kwa maana ya kwamba hawabadiliki kulingana na mazingira pamoja na wakati, na hudumu katika tabia zao zilezile. Hawa huwa ni wahusika wa kiidili, hubeba matarajio ya mwanajamii bora. Pamoja na upungufu wa wahusika bapa wakiwamo wahusika wakweza, wahusika hawa huwa ni muhimu kwa kufunza maadili mema kwa wanajamii. Wahusika wa hadithi fupi andishi zote zilizochunguzwa ni wahusika mviringo kwa kuwa wanabadilika kimtazamo, kisaikolojia na kitabia kulingana na mazingira pamoja na wakati. Jambo hilo linaleta taksiri katika kufundisha mwenendo mwema unaohitajika katika jamii.

Iribemwangi (2000) na Ngure (2003) wanaeleza kuwa wahusika wa hadithi fupi ni wachache na hawajaelezwa kwa mapana zaidi. Hoja hii ya wahusika imefafanuliwa katika Samwel (2012:43-44) kuwa hadithi fupi za sasa zimekiuka dai hilo, ijapokuwa idadi ya wahusika kuwa wengi haijulikani ni kuanzia wangapi. Wahusika katika hadithi fupi tulizozichunguza katika magazeti teule ni wengi, kwa mfano, hadithi ya *Aliyevaa Ngozi ya Kondoo* katika *Nipashe* ina wahusika 17 wafuatao: Mahirane, Jacob, Mzee Njenje, Mzee Mbenzi, Msoka, Bi Matesha, Magosho, Ngogomi, Siti Ally, Ngumbili, Ngomani, Mbilinyi, Machange, Manyanga, Abunaya, Mavura na Fundi Viatu. Suala la wahusika kutoelezwa kwa mapana nalo halihalisiki katika hadithi fupi za sasa. Kwa mfano, katika hadithi ya *Utata Mtupu* wahusika Herrieth na Frank wameelezwa kwa kina, hususani kuhusiana na maumbo yao, tabia zao na maeneo walikozaliwa na kukulia.

Wahusika wa hadithi fupi za mwanzo walikuwa wahusika bapa vielelezo kwa maana ya kwamba majina yao yaliendana na tabia zao. Pia, wahusika wanyama majina yao yalikuwa yakijulikana kwa tabia fulani. Senkoro (2011) anafafanua kuwa wahusika wanyama walihitajika wawakilishe tabia, mienendo na matendo ya watu halisi. Anaeleza kuwa kwa Afrika Mashariki yote sungura anajulikana kwa

tabia ya ujanja, fisi anawakilisha tabia ya uchoyo na ulafi, bundi huashiria mabaya na kifo, tausi husimamia uzuri na maringo, nzige huwakilisha njaa, uroho na ulafi na kobe hujulikana kwa busara na hekima. Senkoro (*khj*) anaeleza zaidi kuwa, wahusika hawa walitumiwa katika hadithi kwa kutegemea eneo la kijiografia. Wahusika katika hadithi fupi andishi 13, kati ya 16 tulizozichunguza, majina yao hayakuonekana kuwakilisha au kuendana na tabia au mienendo yao. Uteuzi wa majina yao, wala haukuzingatia maeneo wanayotoka. Kwa mfano, katika hadithi ya *Siku za Mwizi* iliyoandikwa na Saidi katika *Nipashe* tar. 20-22/2/2008, tunawaona wahusika watatu waliojitokeza sana Zena, Jimmy na Mary. Zena anajitambulisha kama mtu wa Tanga, huyu ni mwanamke mwenye tamaa asiyeweza kuzuia hisia zake. Jimmy ni mwanamume mwenye tabia ya usaliti katika ndoa yake na Mary ni mwanamke asiyeweza kutunza siri za ndoa yake. Majina haya hayaendani kabisa na utamaduni wa Waswahili na tabia za wahusika katika hadithi nzima.

Majina ya wahusika na tabia zao havichukuani na utamaduni wa asili wa Waswahili. Majina ya wahusika kwa sehemu kubwa yana asili ya jamii za mataifa ya Kimagharibi na Mashariki ya Kati. Halikadhalika, tahajia za majina hayo zimefuata lugha ya Kiingereza na ya Kiarabu. Kwa mfano, katika hadithi ya *Utata Mtupu* inayohusu vijana kuchanganya mapenzi na shule ina wahusika wafuatao: Ashura, Herrieth, Dennis, Frank, Mzee Dumisani, Satty, Amin, Loveness na Caroline. Pia, hadithi ya *Kwa Nini Mimi?* iliyoandikwa na Shoko katika gazeti la *Mwananchi* la tar. 3-5/11/2008 inayohusu visa vya kimapenzi ina wahusika Ashura, Irene, Glory, Emanuel, Neema, Mwanaidi na Chriss. Aghalabu majina ya wahusika wa hadithi fupi za kipindi kabla ya utandawazi yalikuwa na maana inayoendana na maudhui ya hadithi. Majina ya wanyama, kwa mfano, fisi mwenye sifa ya uroho yalitumiwa katika matukio yanayoendana na tabia hiyo. Kutajwa kwa jina peke yake kilikuwa ni kipengele kimojawapo cha uzuri katika hadithi inayosimuliwa kwa kuwa wasikilizaji walikuwa wakirejelea tabia zinazoambatana na jina hilo. Makala hii imebaini kuwa katika hadithi fupi andishi za magazeti yaliyochambuliwa hakuna uhusiano wa jina kama la Frank na vitendo vya uasherati alivyokuwa akivifanya. Hapa inaonyesha wazi kuwa majina haya ya wahusika yametumiwa kwa lengo la kukidhi haja ya usasa, ni majina yanayokwenda na wakati. Haya ni majina yanayotumiwa na jamii mbalimbali za ulimwengu. Kubadilika kwa majina ya wahusika na matumizi yake ni ushahidi wa wazi wa kukengeuka kwa ujumi wa Kiafrika.

Kasumba ya waandishi na jamii kwa jumla ya kupenda majina ya kigeni yenye asili ya utamaduni wa Kimagharibi ni uthibitisho mzuri unaoonyesha kuwa masuala ya Kimagharibi yana nafasi kubwa katika hadithi fupi andishi za kipindi hiki cha utandawazi. Kwa jumla hoja hizi zinathibitisha kuwapo kwa athari za

mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika kipengele cha wahusika katika hadithi fupi andishi za Kiswahili.

**3.4 Kutokuzingatiwa kwa Msuko Asili wa Hadithi Fupi**

Msuko ni kipengele kimojawapo cha upande wa fani katika kazi ya fasihi. Mtunzi hutumia mbinu mbalimbali za kiufundi katika kulisana umbo la kazi ya fasihi ili iwe na mvuto kwa hadhira, na hii huwa ni hatua mojawapo ya kukidhi mahitaji ya kiujumi katika kazi ya fasihi. Msokile (1992) na Iribemwangi (2000) wanaeleza kuwa hadithi fupi inapaswa iwe na msuko ambao ni sahili. Huu ni usimulizi wenye mpangilio mzuri wa maelezo yanayotiririka kutoka mwanzo hadi mwisho wa kutendeka kwa kadhia. Samwel (2012:41-42) akihakiki hoja ya wataalamu hawa anahoji kuwa, kwa kuwa hadithi nyingi za sasa hazifuati huo mtiririko sahili, je, tusiziite hadithi fupi? Samwel anafafanua kuwa sifa hiyo pengine ilikuwa mwafaka kwa hadithi fupi simulizi za kimapokeo. Baadhi ya hadithi fupi andishi za sasa hazifuati mtiririko sahili wa matukio ambayo yanasimuliwa bila kufuata mpangilio mzuri. Sehemu ya kati ya hadithi inaweza kuanza na iliyopaswa kuwa mwanzo inaweza kuwa mwisho. Madumulla (2009) anaeleza kuwa msuko ni mtiririko wa matukio katika hadithi kiusababishi. Msanii mzuri ni yule anayepanga kazi yake kiasi kwamba tukio moja likasababisha jingine, hii hujenga hamu ya msomaji ya kutaka kuendelea kujua kulikoni. Tunaweza kujiuliza kwa nini hadithi fupi za kimapokeo zilitumia mtiririko sahili tu na za sasa zina uhuru wa kutumia mtiririko wowote wa matukio. Jambo mojawapo linalotofautisha hadithi za kimapokeo na za sasa ni uwingi wa visa vinavyojenga hadithi. Hadithi fupi za sasa zinajengwa na visa vingi, jambo linalorahisisha kuwapo na msuko changamani wa matukio.

Hadithi fupi ya *Utata Mtupu* imeanza kwa kueleza maisha ya Herrieth akiwa amemaliza elimu ya chuo kikuu na kuajiriwa na shirika moja la kimataifa na huku akiwa anaendelea na uhusiano na Frank kama mume wake. Herrieth baada ya kumfumania Frank kwenye chumba alichompangishia Sinza, anapigwa na Frank na wanavunja mahusiano. Baada ya Herrieth kutibiwa majeraha yaliyosababishwa na kipigo kutoka kwa Frank anarejea kwa wazazi wake. Hapo ndipo tunaelezwa maisha yao wakiwa chuo na namna Frank na Herrieth walivyoanza mahusiano. Hatimaye tunaelezwa juu ya marafiki wa Frank na Herrieth wakijitahidi kusaidia kurejesha mahusiano yaliyovunjika. Wakati huo Frank alikuwa amelazwa hospitalini Temeke baada ya kupoteza fahamu kutokana na kukabiliwa na msongo wa mawazo. Mtiririko wa visa katika hadithi hii ni kwamba sehemu iliyopaswa kuanza imekuwa kati na sehemu ya kati imekuwa mwanzo. Uchangamani wa visa pia umejitokeza katika hadithi ya *Sitakusahau Mpenzi Wangu Anita* ya tar. 17-20/10/2011 na hadithi ya *Dereva wa Taksi* ya tar. 5-10/1/2010 zote zimeandikwa na Mustafa katika gazeti la *HabariLeo*.

**3.5 Taksiri katika Upokezi wa Utanzu**

Riwaya ya Kiswahili ni utanzu wenye ufanano wa karibu sana na hadithi fupi andishi za Kiswahili. Asili ya utanzu wa riwaya ni kutoka katika jamii za mataifa ya Kimagharibi. Hadithi fupi simulizi zilizokuwa zikihifadhiwa kichwani, ziliwekwa katika maandishi baada ya kupatikana kwa teknolojia ya maandishi. Hilo likasababisha utanzu wa hadithi fupi andishi kuchukua nafasi ya utanzu wa hadithi fupi simulizi. Utanzu wa hadithi fupi andishi kwa kuwa ni mbadala wa hadithi fupi simulizi ulipaswa kuendelea kupewa nafasi kubwa katika jamii kuliko hata riwaya kwa sababu una nasaba na utamaduni wa Kiafrika.

Makala hii imebaini kuwa jamii ya watu wa vijijini tangu kuingia kwa maandishi, utanzu wa hadithi fupi umetoweka kwa wanajamii. Wanafunzi wanaosoma ndiyo angalau kwa sehemu huzisoma hadithi fupi katika somo la Kiswahili. Vijiji vingi bado havijafikiwa na nishati ya umeme hivyo inakuwa ni vigumu kufikiwa na hadithi fupi zinazotambwa katika televisheni. Magazeti ambayo ni chombo ambacho waandishi wengi wa hadithi fupi wamekuwa wakitumia kuchapisha hadithi walizoandika, bado yanaishia sehemu za mijini, hayafikishwi vijijini. Hivyo, kuna utengano mkubwa wa hadithi fupi andishi na jamii ya watu wanaoishi katika vijiji vya pembezoni.

Katika hadithi fupi teule zilizochunguzwa katika magazeti ya *HabariLeo*, *Nipashe* na *Mwananchi*, imeonekana kuwa hadithi fupi andishi za sasa zinazochapishwa magazetini zimewabagua wanajamii. Maudhui, lugha na picha zinazochorwa vinaendana na rika la vijana. Masuala yanayozungumzwa katika hadithi hizo kwa sehemu kubwa yanahusiana na harakati za mapenzi ya vijana wa mijini. Watu wenye umri mkubwa waishio mijini hawavutiwi na hadithi hizo kwa kuwa zinaonekana kuwalenga vijana. Hadithi hizo zinaonekana kukiuka maadili ya Kiafrika kwa kuwa masuala yanayotakiwa kuelezwa kwa kificho yanaongelewa waziwazi. Pia, mandhari na matukio yanayowahusu watu wa vijijini nayo hayajapewa nafasi katika hadithi hizo. Hivyo, pamoja na kwamba kupatikana kwa magazeti vijijini ni nadra bado hadithi fupi zinazoandikwa katika kurasa za magazeti hayo hazina mvuto kwao kwa kuwa zimesawiri uhalisi wa mijini.

Ufundishwaji na usomaji wa hadithi fupi andishi katika taasisi za elimu nao umekuwa na changamoto zake. Samwel (2012:72) anaeleza kuwa nchini Tanzania wanafunzi wa sekondari hawafundishwi kabisa utanzu huu. Wanasoma tanzu za riwaya, ushairi, tamthiliya na kidogo fasihi simulizi ilhali utanzu wa hadithi fupi andishi wakati mwingine hautajwi kabisa. Baadhi ya vyuo vikuu hufundisha utanzu wa hadithi fupi andishi, lakini vingine huuchukulia utanzu wa hadthi fupi andishi kama sehemu ya riwaya. Kwa mfano, katika Mtaala wa Chuo Kikuu cha Dodoma

ya 2018/2019 unaopatikana katika www.udom.ac.tz ukurasa wa 48 kuhusu kozi za fasihi andishi kuna kozi ya riwaya (KF 220), tamthiliya (KF 221), ushairi (KF 210) na Fasihi ya Kiswahili na Urithi wa Masimulizi (KF 212), hakuna kozi ya hadithi fupi andishi. Hadithi fupi andishi hazitajwi mahali popote labda hufikiriwa kuwa ni sehemu ya riwaya.

Tangu kipindi cha awali ambacho jamii za Kiafrika zilikuwa bado hazijachangamana na jamii za mabara mengine hadi sasa, shughuli za uzalishaji mali zimekuwa na athari kubwa katika ustawi na maendeleo ya hadithi fupi. Kipindi hicho hadithi zilisimuliwa wakati wa jioni baada ya kazi na wanajamii walikusanyika mahali pamoja. Ilikuwa ni nadra kwa mtu mmoja au wawili kutamba hadithi peke yao kwa kuwa ushiriki wa hadhira ulikuwa na umuhimu mkubwa kiujumi. Shughuli za uzalishaji mali za kipindi hicho cha awali zilikuwa zikifanyika kwa umoja. Hata fasihi nayo iliakisi hali hiyohiyo. Siku hizi watu hawaishi maisha ya ushirika kama mwanzo, sehemu kubwa ya watu wamehama katika maeneo ya vijijini na kwenda mijini kufanya kazi mbalimbali. Usimuliaji wa hadithi ama umepungua au umeisha kwa kuwa maisha yale ya mwanzo hayapo tena. Hadithi zimehamia katika maandishi ambapo msomaji wa hadithi fupi huhitaji muda wa faragha ili kuburudika na hadithi anayoisoma. Usomaji huo hufanyika muda wowote ilimradi kazi zikipungua. Hata hivyo, jamii ya watu wa mijini ndiyo inayobahatika kuyapata magazeti na kuzisoma hadithi fupi. Watu wanaoishi pembezoni mwa miji hawafikiwi na magazeti, hivyo, kukosa nafasi ya kufikiwa na hadithi hizo ijapokuwa baadhi yao, kazi wanazozifanya zinawapa nafasi ya kusoma magazeti. Utanzu wa hadithi fupi (simulizi na andishi) kwa jamii ya watu wanaoishi vijijini ni kama umekufa kwa sababu ya kukosekana kwa nishati ya umeme katika maeneo mengi ya pembezoni. Hii huwanyima nafasi ya kuona na kusikiliza hadithi fupi zinazotambwa kwenye televisheni. Redio ni chombo mwafaka kwa watu wa vijijini lakini redio nyingi hazina vipindi vya simulizi za hadithi fupi. Vipo vipindi kwenye redio ambavyo hujaribu kila siku asubuhi kuelezea yaliyojitokeza magazetini lakini hadithi fupi huwa haziguswi kabisa. Watoto wanaosoma shule za msingi na vijana wanaosoma shule za sekondari angalau wana nafasi ya kuzisoma hadithi fupi zile zilizoandikwa kwenye vitabu vya kiada na ziada.

Utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili umeathirika kwa kiasi kikubwa kwa kukengeushwa kwa ujumi wa Kiafrika na masuala mbalimbali ya kiutandawazi kiasi cha kukosa mvuto katika jamii. Ipo hatari ya utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili kupotea kama jamii haitachukua jitihada za kuupa nafasi ya kutosha.

### 3.6 Kubadilika kwa Njia za Kuhifadhi na Kuwafikia Hadhira

Athari katika njia za kuuhifadhi utanzu wa hadithi fupi andishi zinajitokeza katika pande mbili, upande hasi na upande chanya. Tukianza na upande chanya ni kwamba

maendeleo ya kiteknolojia ya kipindi cha utandawazi yameufanya utanzu wa hadithi fupi andishi uhifadhiwe kiurahisi katika njia mbalimbali na kuwafikia wasomaji katika njia mbalimbali. Hadithi fupi za sasa zinaweza kusomwa katika vitabu, magazeti, intaneti, simu, kusikilizwa na kuonwa katika televisheni. Mwanzoni hadithi fupi zilikuwa zinahifadhiwa katika vichwa vya watambaji na kutambwa katika eneo dogo la jamii. Baada ya kuja teknolojia ya maandishi hadithi fupi zimekuwa zikihifadhiwa na kuifikia hadhira kwa njia ya magazeti na vitabu, hivyo, eneo la jamii linalofikiwa na utanzu likaongezeka. Katika ipindi hiki cha utandawazi vifaa vya kisasa vya kuhifadhia na kusambaza hadithi fupi vipo katika mfumo wa kielektroniki ambapo utanzu huu unawafikia wasomaji kwa urahisi na kwa muda mfupi katika dunia nzima. Vikwazo vinavyosababishwa na tofauti za lugha za jamii za mataifa hutatuliwa kupitia tafsiri ambayo inafanyika kiotomati kupitia mifumo ya mawasiliano ya kielektroniki. Kutokana na athari za mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi andishi uliosababishwa na maendeleo ya kiteknolojia, hadithi fupi andishi za Kiswahili zimekuwa na sura ya fasihi ya dunia kifani na kimaudhui. Hivyo, maendeleo ya kiteknolojia katika kipindi cha utandawazi yameongeza kasi katika mabadiliko ya idili za jamii ya Kiafrika juu tathmini ya ujumi katika kazi zao za Fasihi.

Upande wa athari hasi za mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika uhifadhi na namna hadithi fupi andishi zinavyowafikia wasomaji, unahusiana na udhibiti pamoja na miundombinu. Udhibiti wa hadithi fupi andishi ambazo zinatumia lugha isiyo ya staha na kueleza masuala yanayokiuka maadili ya jamii ya Watanzania unakuwa mgumu. Mijongeo ya vitu, taarifa pamoja na fasihi katika mifumo ya kielektroniki kati ya jamii za kimataifa, uratibu wake huwa mgumu. Kwa mfano, katika hadithi ya *Siku za Mwizi* mhusika Zena anaeleza namna alivyomshawishi Jimmy kufanya ngono, anasema:

> Nami siku hiyo nilimpania kumwonyesha au kumpa mapenzi yanayowafanya wanaume wengi wachanganyikiwe kutoka kwa wanawake wa Kitanga. ...niliupandisha mkono wangu mpaka kwenye chuchu zake za kiume zilizodundumaa na kuzichezea chezea kiaina. Nikakuta anapandisha pumzi na kuzishusha kwa nguvu nikajua tayari, Jimmy kwisha habari yake... Shhhhh! Nikajifanya kuonja mchuzi ili nizidi kumchanganya. Nikajilaza mapajani mwake, nikaanza kufungua mlango wa ikulu, kilichofuata ni kulamba koni kwa ulimi. Niko hoi taabani sijiwezi alisema huyu mwanaume (*Nipashe*, 21/02/2008).

Dondoo hili linaonesha wazi ukiukaji wa maadili ya Kitanzania kwa kueleza vitendo vya kingono waziwazi. Katika utamaduni wa Kiafrika masuala haya yaliongelewa jandoni na unyagoni na mahali pengine pa faragha. Lakini katika nyakati hizi za utandawazi yazungumzwa na kuoneshwa kila mahali kwa uwazi.

Njia za kisasa za uhifadhi wa hadithi fupi zinauweka utanzu huu kwenye hatima inayotia mashaka kuhusu uhai wake. Imeonekana wazi kuwa utanzu huu unapohifadhiwa katika maandishi unachukua sura inayokaribia kufanana na riwaya. Kwa mfano, kuna baadhi ya wataalamu wanaozichukulia hadithi fupi kama kajitanzu ndani ya utanzu wa riwaya (taz. Samwel, 2012). Hoja zinazoelezwa ni kwamba sifa za hadithi fupi andishi za sasa na za riwaya kwa kiasi kikubwa zinafanana. Sifa za riwaya kama za kuwa na mchangamano wa visa vingi, wahusika wengi, kuwa zao la kibepari na suala la uhuru pia ndizo sifa zinazobainika katika hadithi fupi andishi za sasa. Hadithi fupi zinaposimuliwa katika televisheni kwa kuonyeshwa na matendo kadhaa ya wahusika, huchukua umbo la kitamthiliya. Pamoja na hayo, sifa na vionjo vingi vya awali vya utanzu huu vilivyoambatana na umbo lake la usimulizi vimepotea kwa sababu ya mabadiliko yanayotokea wakati wa uhifadhi.

### 3.7 Mkanganyiko katika Mitazamo kuhusu Utanzu

Elimu ni mojawapo ya nyenzo zenye athari na mchango mkubwa katika kukengeusha ujumi wa Kiafrika katika kazi za fasihi za Waafrika. Kumekuwa na kasumba ya wasomi wa Kiafrika kutumia kazi za fasihi za Kimagharibi kama kipimo cha kutambua ubora wa kazi za fasihi za Kiafrika. Utanzu wa hadithi fupi andishi umekuwa ni miongoni mwa tanzu za fasihi ya Kiswahili ulioibua mijadala na mikinzano mingi. Kwa mfano, kuhusu jina la utanzu; wapo wanaoona ingefaa uitwe hadithi fupi za kisasa, wengine wanaona uitwe riwaya fupi (taz. Madumulla, 2009; Samwel, 2012). Kutokana na kujiegemeza mno katika mitazamo ya Kimagharibi katika kuhakiki kazi za Kiafrika, wapo wataalamu wanaoona kazi za Fasihi za Kiafrika ni chapwa hususani riwaya kwa sababu maudhui, wahusika, muktadha na matukio huwa vinakosa uhalisi. Uhakiki wa namna hiyo unakuwa haujazingatia maisha halisi ya Waafrika kwa sababu kazi nyingi za fasihi ya Kiafrika hupata fasiri baada ya kuhusianisha ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Utandawazi umefifisha kwa sehemu kubwa kiwango cha ubunifu cha Waafrika kutokana na kuiga masuala ya kigeni ambayo hayahalisiki katika muktadha wa jamii za Kiafrika.

Mwandishi wa makala hii alifanya mahojiano na wakazi wanaoishi katika vijiji vya wilaya ya Makete, kwa lengo la kujua hali ya utambaji wa hadithi katika maeneo yao, kwa kuwa vijiji hivyo bado havijafikiwa na umeme. Miundombinu ya umeme ni ya msingi kwa ajili ya kuwezesha vifaa vya kisasa vya mawasiliano

kufanya kazi. Wahojiwa hao walijibu kuwa utambaji wa hadithi haufanyiki tena hata kama televisheni hazijawafikia katika vijiji vyao. Kwa mfano, Bwana George Ngulwa mkazi wa kitongoji cha Ng'ondong'i, anayejulikana kwa lakabu ya 'Kɨswahɨli' alisema:

> Siku hizi hadithi hazisimuliwi kama zamani, sisi wazee tumeacha kabisa, hatusimulii. Serikali imeliondoa jukumu hilo kutoka kwetu na kuwapatia walimu wanaotufundishia watoto wetu shuleni. Hadithi hizo zimeandikwa kwenye vitabu na walimu ndio huwaongoza watoto kuzisoma, sisi kwa sasa tumepumzika. Hata ningewaita wajukuu zangu niwasimulie hadithi hawawezi kunisikiliza, kitakuwa ni kitu kigeni kwao. Ila tunaiomba serikali watumie hadithi zetu za zamani zilikuwa zinafundisha mambo yenye akili (mazuri) (Mahojiano ya tarehe, 07/12/2016).

Elimu ya sasa ni nyenzo mojawapo ya kiutandawazi iliyohusika kukengeusha ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi. Hadithi zilizoandikwa vitabuni zinaposomwa au kufundishwa na walimu shuleni huwa tayari zimepungukiwa mambo kadhaa yaliyokuwapo kwenye hadithi fupi simulizi: Kwanza, kipengele cha mandhari ya hadithi huwa kimepuuzwa. Hadithi inayohusu kisa cha uvuvi husomwa na wanafunzi wote hata wale waliokulia kwenye maeneo yasiyozungukwa na mito mikubwa, bahari na mabwawa. Wakati mwingine hadithi zinazungumzia matukio katika mandhari za mjini na wakalazimishwa kuzisoma wanafunzi wa vijijini. Hali hiyo, hupunguza uwezo wa akili zao wa kujenga taswira kwa kile wanachokisoma. Pili, hadithi zinazosomwa darasani huwa ni rasmi mno kiasi cha kuondoa hali ya burudani kwa kuwa huambatana na maswali pamoja na majaribio. Tatu, nafasi ya mwalimu wakati wa usomaji na ufafanuzi wa hadithi inaweza isiwe na ufanisi kwa sababu ya kutokuufahamu vizuri utamaduni wa jamii husika.

Utandawazi umechangia kuenea kwa dini za Kimagharibi ndani ya jamii za Kiafrika wakati dini za jadi zikififishwa. Ni dhahiri kuwa imani za dini za jadi zilichukua nafasi kubwa katika kazi za sanaa za Kiafrika. Wahusika wengi wa kingano walikuwa ni majitu yenye sura na uwezo wa kimiungu. Imani za dini za kijadi zilikuwa ni kipengele kimojawapo cha ujumi katika kazi za fasihi hususani hadithi fupi simulizi. Usasa kupitia imani za dini za Kimagharibi umebadilisha mitazamo ya Waafrika kuhusu dini zao za asili, imani za dini za jadi zimeonekana ni za kishetani. Jambo hili linathibitika hata katika hadithi 16 zilizochambuliwa na mwandishi, ni hadithi moja tu ya *Harufu ya Mauti* iliyoandikwa na Chuma tar. 17-28/8/2010 katika gazeti la *Mwananchi* ndiyo iliyozungumzia masuala ya imani za dini za jadi na uzuri wake. Ijapokuwa Waafrika walio wengi wanaonekana kukosa ujasiri wa kuendeleza imani zao za asili kwa uwazi, wapo wanaoendelea na imani

hizo kwa kificho. Mwandishi Abdallah katika hadithi ya *Vituko* iliyochapishwa katika gazeti la *HabariLeo* tar. 4-7/4/2011 anashadidia kuwa bado wapo watu wanaozienzi dini za asili kwa kificho. Anamtumia Mama Zaituni, mhusika ambaye ni mfano mzuri wa watu hao, yeye alikuwa akienda kwa mganga wake wa kienyeji kuchukua dawa zitakazowezesha mipango yake ifanikiwe, ikiwa ni pamoja na kupandishwa cheo kazini. Imani za dini ni za muhimu katika ustawi wa maisha ya jamii yoyote ile ulimwenguni. Yapo masuala magumu ambayo ufumbuzi wake huwa haupatikani kupitia maarifa ya kawaida ya akili ya binadamu pamoja na sayansi. Utatuzi wa masuala hayo huwa ni kwa kupitia imani za dini pekee. Imani za dini za Kimagharibi zinapoonekana kushindwa kutoa majibu au utatuzi wa masuala yanayowasumbua Waafrika, ndipo huzigeukia imani za asili au kuchanganya imani za dini za kijadi na za Kimagharibi.

Kwa ujumla, mitazamo ya wanajamii iliyobadilishwa na elimu pamoja na dini za Kimagharibi imeathiri mitazamo yao juu ya hadithi fupi andishi za Kiswahili. Hadithi fupi andishi zinatathiminiwa kwa kulinganishwa na kazi za fasihi za mataifa ya Kimagharibi. Jambo hilo huwafanya waandishi kujiingiza kuandika masuala mtambuka ya kidunia, ambayo wakati mwingine yanakuwa hayana mizizi katika jamii yetu. Hali hii pia inatweza kukua kwa uwezo wa kiubunifu wa wasanii wetu. Kwa kuwa huamini kuwa ili kazi za sanaa za Waafrika zionekane kuwa bora, hapana budi kuzifinyangafinyanga hadi zifanane na zile za Kimagharibi.

## 4.0 Hitimisho

Ujumi wa kisanii katika fasihi umefungamana na jamii inayotumia fasihi hiyo. Ieleweke kuwa ujumi unajumuisha hisia zinazohusiana na uzuri au ubaya, ubora au uduni, ladha na thamani za kazi za sanaa. Hivyo, kukengeuka kwa ujumi wa Kiafrika kunaleta mabadiliko katika kutazama ubora, thamani na uzuri katika kazi za fasihi zikiwamo hadithi fupi andishi za Kiswahili. Miongoni mwa mambo yanayokengeusha ujumi wa Kiafrika ambayo makala hii ilimakinikia ni utandawazi. Athari za mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi andishi zilizoibuliwa na kuelezewa na makala hii ni: Mosi, kuwapo kwa maudhui mapya katika utanzu huu. Pili, kufifishwa kwa utambulisho wa utanzu huu. Tatu, mabadiliko katika wahusika na usawiri wa wahusika. Nne, mabadiliko katika msuko wa matukio kutoka ule wa asili uliozoeleka wa mtiririko wa mwanzo, kati na mwisho. Tano, mwitikio wa hadhira kuhusiana na utanzu wa hadithi fupi andishi za kipindi cha utandawazi umekuwa tofauti na wa hadithi fupi simulizi kabla ya utandawazi. Sita, mkengeuko huo wa ujumi umeathiri uhifadhi na ufikiwaji wa hadithi fupi andishi katika jamii, na mwisho kuwapo kwa mkanganyiko ya kimitazamo kuhusiana na utanzu huu.

Maoni yetu ni kwamba, endapo utanzu wa hadithi fupi andishi za Kiswahili hautapata nafasi katika jamii kama ile ambayo utanzu wa hadithi fupi simulizi ulipata kabla ya kipindi cha utandawazi, kuna hatari ya utanzu huu kupotea au kumezwa na riwaya. Asili ya utanzu wa riwaya ni kutoka katika jamii za mataifa ya Kimagharibi. Ifahamike kuwa hadithi fupi simulizi zilizokuwa zikihifadhiwa kichwani, ziliwekwa katika maandishi baada ya kuja kwa teknolojia ya maandishi. Jambo hilo likasababisha utanzu wa hadithi fupi andishi kuchukua nafasi ya utanzu wa hadithi fupi simulizi. Utanzu wa hadithi fupi andishi kwa kuwa ni mbadala wa hadithi fupi simulizi ulipaswa kuendelea kupewa nafasi kubwa katika jamii kwa sababu una nasaba na utamaduni wa Kiafrika. Utanzu huu unapaswa kupewa uzito wa kipekee na wadau wote wa fasihi pengine kuliko utanzu wa riwaya kwa kuwa bado una nafasi kubwa ya kuisaidia jamii ya Waswahili kutokana na sifa yake ya kueleza mambo kwa muhtasari au mbano. Wanajamii wa sasa wanakimbizana na shughuli mbalimbali za maisha, hawana nafasi ya kusoma hadithi ndefu kama za riwaya, hadithi fupi zingetumiwa vizuri zingeweza kuwa mwafaka kwa jamii yetu katika kipindi hiki cha utandawazi.

**Marejeleo**


Dollar, D. na Kraay, A. (2001a). *Growth is Good for the Poor, mimeo: Development Research Group.* Washington: The World Bank.

Iribemwangi, P.I. (2000). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.* Nairobi: East Africa Educational Publishers Limited.

Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Dar es Salaam: Mture Educational Published Limited.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phonex Publishers.

p'Bitek, O. (1972). *Song of Lawino and Song of Ocol*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Limited.

Samwel, M. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia, Mbinu na Mifano*. Iringa: Kasenyenda Tanzania.

Samwel, M. (2013). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: Meveli Publishers.

Sanga, A. N. (2018). Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano ya Hadithi Fupi kutoka Magazeti ya *HabariLeo, Nipashe* na *Mwananchi* ya Mwaka 2008

Hadi 2014, Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Shepard, B. na Hayduk, R. (Wah.) (2002). *From ACT UP to the WTO: Urban Protest and Community Building in the Era of Globalization*. London: Verso.

Wamitila, K. W. (2010). *Wali wa Ndevu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Vide – Muwa.

Waters, M. (2001). *Globalization*. London: Routledge Taylor and Francis Group.